

# **AMIRUL MUUMININA NA MAKHALIFA**

**Kimeandikwa Na:**

Ustadh Ahmad Mustafa Yaaqub

**Kimetarjumiwa na:**

Abdul Karim Juma Nkusui

ترجمة

أمير المؤمنين عليه السلام  
والخلفاء

تأليف  
أحمد مصطفى يعقوب

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:  
AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 - 512 - 08 - 9

**Kimeandikwa na:**  
Ustadh Ahmad Mustafa Yaaqub  
**Barua Pepe:** Tanwerq8@hotmail.com

**Kimetarjumiwa na:**  
Abdul Karim Juma Nkusui  
**Barua pepe:** abdulkarimjuma@yahoo.com

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**  
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Juni, 2013  
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**  
Alitrah Foundation  
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania  
**Simu:** + 255 22 2110640 / 2127555  
**Barua Pepe:** alitrah@raha.com  
**Tovuti:** www.ibn-tv-com  
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Amesema Mwenyezi Mungu (swt): “**Alif lam raa, kitabu tumekiteremsha kwako ili uwatoe watu katika giza kwenda kwenye nuru kwa idhini ya Mola wao katika njia Mwenye nguvu Mwenye kuhimidiwa**” (Sura Ibrahim: 1).

Amesema Mwenyezi Mungu (swt): “**Je, Mwenye kuongoza katika haki ana haki zaidi ya kufuatwa au asiyeongoza hadi aongozwe? Vipi mnahukumu**” (Sura Yunus: 35).

Amesema Mwenyezi Mungu (swt): “**Je wanalingana wenye kujua na wale wasiojua? Hakika wenye kukumbuka ni wale wenye akili**” (Sura Zumar: 9).

---

# **YALIYOMO**

---

Neno la Mchapishaji.....	06
Utangulizi .....	08
<b>Sehemu ya Kwanza .....</b>	<b>11</b>
Wingi wa Elimu ya Amiril-Muuminina ('as) Mbora kushinda watu wote wa Madina .....	11
<b>Mlango wa Pili.....</b>	<b>28</b>
Kati ya Amirul-Muuminina ('as) na Abu Bakr.....	28
<b>Mlango wa Tatu .....</b>	<b>31</b>
Kati ya Amirul-Muuminina ('as) na Umar bin al-Khattab .....	31
<b>Mlango wa Nne .....</b>	<b>39</b>
Baina ya Amirul-Muuminina ('as) na Uthman bin Affan. ....	39
<b>Mlango wa Tano.....</b>	<b>41</b>
Baina ya Amirul-Muuminina ('as) na Mu'awiya.....	41
<b>Mwisho .....</b>	<b>45</b>
<b>Bibliografia.....</b>	<b>47</b>
Orodha ya Vitabu viliyvo chapishwa na Al-Itrah Foundation .....	49

## NENO LA MCHAPISHAJI

**K**itabu ulilchonacho mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, *Amiru l-Mu'miniin 'Alaysi 's-Salaam wa l-Khulafaa'* kilichoandikwa na Ustadh Ahmad Mustafa Yaaqub. Sisi tumekiita, *Amirul Muuminina na Makhalifa*.

Kitabu hiki kinazungumzia ubora, hekima, busara, ushujaa, uadilifu na elimu ya Imam Ali (a.s.). Kila Mwislamu na asiyeh Mwislamu ambaye amesoma histofia ya Uislamu na ambaye hana upendeleo wala chuki, atakubaliana na sifa zilizoainishwa hapo juu kwamba zote hizo anazo Imam Ali (a.s.) na kwamba yeeye ndiye mwenye kustahiki sifa hizo zaidi baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), kama alivyosema mwandishi katika utangulizi wake. Hatusemi kwamba wen-gine hawana sifa hizo, bali tunasema aliye na sifa hizo zaidi ni Imam Ali (a.s.).

Mwandishi wa kitabu hiki amefanya utafiti wa kina katika maeneo yote yaliyotaja ya sifa hizo kwa kutumia vyanzo vyingi k.v. Qur'ani Tukufu, Sunna na vitabu vyta historia ya Uislamu, vitabu vyta hadithi n.k.ili kumpa msomaji kitu kilicho na uhakika kabisa. Basi ungana naye ili uone ni jinsi gani alivyokuwa Imam Ali katika historia ya Uislamu.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana hususan wakati huu ambapo watu wamesoma na akili zao hazikubali tena ngano na hadithi za uwongo na upotoshaji wa historia. Hivyo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa madhumuni yake yaleyale ya ku-wahudumia Waislamu na wasio Waislamu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu Abdul Karim Juma Nkusui kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki pamoja na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

**Mchapishaji  
Al-Itrah Foundation**

---

## UTANGULIZI

---

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

### Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

**S**hukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa Wali-mungu, rehema na amani zimwendee Mbora wa viumbe wote na Bwana wa viumbe Abul-Qasim Muhammad (s.a.w.w.) na Ahali zake wema watoharifu, na laana daima ziwashukie maadui zao na wenyе kukanusha kudhulumiwa kwao, fadhi-la zao na karama zao hadi Siku ya Kiyama.

Ama baad! Akili ya Mwanadamu inaegemea katika kuchagua kilicho bora zaidi na kizuri zaidi. Kwani kuna kizuri na kizuri zaidi, kuna mjuzi na mjuzi zaidi kuna mzuri na mzuri zaidi n.k.

Kwa sababu hiyo Marja'a wetu Mwenyezi Mungu awarehemu wafu kati yao na awadumishe walio hai mionganoni mwao, wametoa fat'wa kuwa ni wajibu kumfuata aliye mjuzi zaidi na kwamba yule asiyemtafuta mjuzi zaidi,<sup>1</sup> na akafuata taqlid aliyoi kuta katika jamii yake, babu zake na baba zake wanaifuata, basi taqlidi yake ni batili na hivyo amali zake zote ni batili, na jambo hili halisemi Ahmad Mustafa kwa sababu yeye si mjuzi, ili wasije wakakasirika wajinga wenyе kasumba

---

<sup>1</sup> Muumini ama atakuwa ni Mujitahid au Muhtat au Muqalid, mwenye kumfuta mjuzi zaidi, na ni wajibu kwa kila Muqalid kumtafuta mjuzi zaidi na sio kufanya taqlid kwa kufuata baba zake, jamaa au mazingira anamoishi.

za upofu na kututuhumu kwa tuhuma batili, bali ni juu ya kila mwenye kufuata taqlid aliyoikuta kwa jamii yake, babu zake na baba zake atafiti na kuuliza maulamaa juu ya usahihi wa taqlid yake ili apate yakini katika moyo wake na akili yake, ili isiwe kama mfano wa wale waliomwambia Mtume wa wenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Haya ndio tumewakuta baba zetu wakiyafuata." Zama hizi ni zama za elimu na teknolojia na wala sio zama za ujahilia ambazo hawa wangali wanaishi humo. Na tunamuomba Mwenyezi Mungu awaongoze na awape tawfiki watubie.

Ama suala la mjuzi zaidi tunesema kwamba akili ya Mwanadamu inaegemea huko, na Shia Imamiyya Al-Ithna Ashariyah ni watu wenye kujali sana nafasi ya akili kinyume na *Ikhbariyah* ambao wamefuta kabisa nafasi ya akili,<sup>2</sup> kwa sababu hiyo Shia lthna Ashariya Al-Imamiya wanaamini juu ya haki ya Imam Ali kwa njia ya nukuu na ya akili, katika upande wa nukuu tunesha zungumzia katika vitabu vyetu viliviyotangulia na muhimu zaidi ni vitabu "*Lam Yasukut*" na "*Baina twalali wa Husein*." Ama katika upande wa akili tunaona kwamba Imam Ali (a.s.) zimetimia kwake sifa za ubora, kwani yeeye ndio shujaa kushinda masahaba wote, mjuzi kushinda wote, mwenye zuhud kushinda wote, mchamungu kushinda wote, mnyenyeketu kushinda wote, mwenye kufahamu kushinda wote na mwenye kujua hukumu kushinda wote.

Katika kijitabu hiki kidogo tunanukuu kutoka katika rejea za Ahlus Sunna tu, (na hili linatupa nguvu katika hoja kwa wapinzani wa Ahhlul bait (a.s.) ) dondoor kutoka katika riwaya

---

<sup>2</sup> Kwa maelezo ya ziada katika maudhui haya rejea kitabu *Haswaadul-Ayaam* cha Sayid Muhammad Bahrul-ulumi au rejea *Kashkuul* cha Ahmad Mustafa ambapo humo tumenukuu ibara za kutoka katika kitabu cha *Haswaadul-Ayaam*.

ambazo zimepokewa juu ya ubora wa Imam Ali (a.s.) katika upande wa kielimu na ujuzi wa hukumu kushinda sahaba wengine wote waliobakia, na hivyo kustahiki ukhalifa bila ya mwingine, vile kama ambavyo kwa muhtasari sana tutazungumzia humo baadhi ya misimamo na mambo ambayo yalitokea baina ya Amirul-Muuminina (a.s.) na Makhalifa, pia ni pamoja na kutosheka na nukuu au kutoa ufanuzi wa baadhi ya nukuu hizo, na hatimaye kuiachia akili ya msomaji mpPENDWA uhuru wa kuchambua.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atukubalie haya machache kwa Qabuli njema kwa baraka ya sala na salamu za Muhammad na kizazi cha Muhammmad. Na tunaomba radhi ikiwa kijitabu hiki kitakuwa na dosari au mapungufu, sawasawa yawe ya uchapishaji au ya kilugha.

*Wanas'alukumu du'a wajazakumullahu khairan.*

---

## SEHEMU YA KWANZA

---

### WINGI WA ELIMU YA AMIRIL-MUUMININA (A.S.)

**Mbora kushinda watu wote wa Madina:**

عن عبد الله وهو ابن مسعود قال: كنا نتحدث أن أفضل أهل المدينة علي بن أبي طالب

**Kutoka kwa Abdillah naye ni Ibnu Mas'ud anasema:  
"Tulikuwa tunazungumza kwamba mbora kushinda watu  
wote wa Madina ni Ali bin Abi Talib."**

Katika maelezo ya pembezoni: Sanadi yake ni sahihi.<sup>3</sup>

**Niulizeni kabla hamjanikosa:**

عن يحيى بن سعيد قال: أراه عن سعيد قال:  
لم يكن أحد من أصحاب النبي (ص) يقول سلوني إلا علي بن أبي طالب

**Kutoka kwa Yahya bin Said anasema: Naona yatoka kwa  
Said amesema: "Hakuwepo yejote kati ya masahaba wa  
Nabii (s.a.w.w.) anayesema: Niulizeni isipokuwa Ali bin  
Abi Talib."**

---

<sup>3</sup> Ahmad bin Hanbal: *Fadhlil Sahaba* Juz. 2 kimehakikiwa na Wasiyullah bin Muhamad Abbas chapa ya daru Ibnil-Jauziy ya Saudia chapa ya tatu 1426H, uk 801–208 Hadith no: 1097

Katika maelezo ya pembezoni: Sanadi yake ni sahihi.<sup>4</sup>

### **Elimu nyingi:**

عن أبي الأسود، قال ابن جريج ورجل آخر عن زاذان قلا: سئل علي عن نفسه فقال:  
إني أحدث بنعمة ربّي، كنت والله إذا سألت أعطيت وإذا سكت ابتدت، فبين الجوانب  
مني علم جم.

**Kutoka kwa Abu Asiwad amesema: Ibnu Jariji na mtu mwininge kutoka kwa Zadhan wanasema: Ali aliulizwa juu ya nafsi yake: Akasema: "Hakika mimi ninawaelezeeni neema za Mola wangu, mimi nilikuwa ninapouliza ninajibii wa na ninaponyamaza ninaanzwa kwa kuulizwa, hivyo ninayo elimu nyingi mno."**

Katika maelezo ya pembezoni: Sanadi yake ni sahihi.<sup>5</sup>

### **Hekima:**

عن حميد بن عبد الله بن يزيد المدنى، أنه ذكر عن النبي قضاء قضى به على بن أبي طالب، فأعجب النبي فقال: الحمد لله الذي جعل فينا الحكمة أهل البيت.

**Kutoka kwa Hamid bin Abdillah bin Yazid Al-Madaniy kwamba yeye alitaja mbele ye Nabii (s.a.w.w.) hukumu aliyoitoa Ali bin Abi Talib. Nabii akastajaabishwa akasema "Alhamdulillahi aliyejalia hekima kwetu Ahlul-bait."**

Katika maelezo ya pembezoni: Malik bin Sulaiman bin Anasi Al-Answariy amesema: Sijamkuta, lakini wengine waliobaki ni wakweli.<sup>6</sup>

<sup>4</sup> Rejea iliyotangulia Uk: 802 Hadith no: 1098

<sup>5</sup> Rejea iliyotangulia Uk: 802 – 803 Hadith no: 1099

<sup>6</sup> Rejea iliyotangulia Uk: 813 Hadith no: 1113

### Dua ya Mtume (s.a.w.w.):

Siitakidi kwamba kuna mtu yejote kutoka katika madhehebu yoyote anakanusha Mwenyezi Mungu kujibu dua ya Nabii wake mtukufu (s.a.w.w.). Kutoka katika rejea za Ahlus Sunna tumekuta hadithi inayoonyesha usahihi wa hukumu ya Imam Ali (a.s.).

**روى النسائي عن حارثة بن مضرب عن علي قال: بعثني رسول الله إلى اليمن، فقلت:**  
**إِنَّكَ تُبَعْثِنِي إِلَى قَوْمٍ هُمْ أَسْنَنُ مِنِّي لَا يُقْضِي بَيْنَهُمْ. فَقَالَ: إِنَّ اللَّهَ سَيِّدُ قُلُوبَكَ وَيَثْبِتُ لِسَانَكَ**

**Nasai ananukuu kutoka kwa Harithah bin Mudhirib kutoka kwa Ali (r.a) kwamba amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alinituma Yemeni na nikasema: Hakika wewe unanitura kwa watu ambao ni wakubwa kwa umri zaidi kuliko mimi ili nikahukumu baina yao. Akasema: Hakika Mwenyezi Mungu ataongoza moyo wako na atathibitisha ulimi wako.”**

Katika maelezo ya pembeni: Sanadi yake ni nzuri.<sup>7</sup>

#### **Kwa nini hakosei?**

Sisi Shia Al-Imamiya al-Ithna Asharia tunaitakidi umaasum wa Imamu Ali (a.s.), kwamba yeye hakosei, na hili bila shaka sio kupetuka mipaka katika kuwapenda Ahlul-bait (a.s.) bali kuna dalili nyingi za kiakili na za nukuu zinazothibitisha hilo, kwa mfano kati ya hadithi za kiakili ni muhalii Mtume kumteua mtu anayekosea kwa sababu atatoa hukumu za dhulma au zinazopingana na sheria ya Kiislamu. Ama dalili za kunukuu riwaya zinatuthibitishia kuwa Amrul-Muumina (a.s.) hatengani

<sup>7</sup> Anasai- Ahmad bin Shuaibu *Khaswaisi Amirul-mumina Ali bin Talibi (as)* kimehakikiwa na Abu Abdallah Al-Amiliy Asalafiy Addaniy bin Munir Aali Zahriy, maktaba ya Asiriya Beirut Uk. 45 Hadith no: 36.

na Qur'ani kwa kauli yake na kitendo chake, kama ambavyo inajulikana kwa kila Mwislamu kwamba Qur'ani tukufu imehifadhiwa kutokana na upungufu na upotevu na Imam kufungamana na Qur'ani tukufu kama inavyoashiria riwaya ambayo tutaitaja inaonyesha juu ya umaasum wa Imam.

al-Hakim an-Nisabury katika *Mustadrak as Sahihain* ameandika kutoka kwa Abu Thabit Maula Abi Dhar kwamba amesema: Nilikuwa pamoja na Ali (r.a) Siku ya Jamali, nilipomuona Aisha amesisima nikaingiwa na lile ambalo huwaingia watu,<sup>8</sup> Mungu akaniondolea hilo wakati wa Sala ya Adhuhuri,<sup>9</sup> ndipo nikapigana pamoja na Amirul Muuminina. Alipomaliza nilikwenda Madina na moja kwa moja nikamwendea Ummu Salamah na kumwambia: Wallahi mimi sijakuja kwa ajili ya kukuomba chakula wala kinywaji, lakini mimi ni huria wa Abu Dhar. Akasema: Karibu sana. Nikamsimulia kisa changu. Akasema: Ulikuwa wapi nyoyo ziliporuka katika mapito yake? Nikasema: Nilikuwa upande ambao Mwenyezi Mungu alinipambanulia wakati wa Adhuhuri. Akasema umefanya vizuri sana, kwani nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema:

علي مع القرآن والقرآن مع علي لن يفترقا حتى يردا على الحوض.

**“Ali yuko pamoja na Qur'ani na Qur'ani iko pamoja na Ali na hawatotengana hadi watakaponijia katika hodhi.”**

Hadithi hii sanadi yake ni sahihi na Abu Said At-Taymiy ndiye yule Aqaiysai, ni mkweli na mwaminifu, lakini (Bukhari na Muslim) hawa jaiandika.

<sup>8</sup> Yaani akapata shaka

<sup>9</sup> Yaani shaka ikamuondoka

Dhahabiy amesema: Ni sahihi na Abu Aqaisai ni mkweli na mwaminifu.<sup>10</sup>

### **Elimu yake ni kutoka kwa Mtukufu Nabii (s.a.w.w.):**

عن عبد الله بن عمرو بن هند الجملي قال: سمعت علياً رضي الله عنه يقول: كنت إذا  
سألت رسول الله أعطياني وإذا سكت ابتدأني

**Kutoka kwa Abdillah bin Amru bin Hindu Al-Jamaly  
amesema: Nilimsikia Ali (r.a) anasema: "Nilikuwa nina-  
pomuuiliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) anani-  
jibu na nikinyamaza ananianza."**

Hadithi hii ni sahihi kwa sharti la Masheikh wawili (Bukhari na Muslimu) na wala hawajaiandika. Dhahabiy amesema kwa sharti la Bukhari na Muslim (ni sahihi).<sup>11</sup>

### **Jiji la Elimu:**

Hadithi: "Mimi ni Jji la elimu na Ali ni lango lake." Ni hadithi mashuhuri sana na ni sahihi, na wametia taukidi ya usahihi wa hadithi hii Maulamaa wengi wa Ahlus Sunna kama vile al-Hakim an-Nisabury na hawajaipinga isipokuwa Nawasibu maadui wa Ahlul- bait (a.s.) kama vile Dhahabiy.

Kuna mmoja wa masheikh wa Kisuni kutoka nchi ya Morocco naye ni Al-Faidh Ahmad bin Muhammad bin Swadiq Al- Hasaniy Al-Maghribiy aliyefariki mwaka 1380, ambaye ni

<sup>10</sup> al-Hakim an-Nisaburiy ni Muhammad bin Abdillah. *Al-Mustadrak Sahihain* Juz: 5 kimehakikiwa na Hamdiy ad Dar Madaash Muhammad ofisi ya Asiriyah Beirut 2006 kitabu *Maarifatu Swahabah* Uk. 17840–1741 Hadith No: 4628

<sup>11</sup> al-Hakim an-Nisaburiy ni Muhammad bin Abdillah. *Al-Mustadrak Sahihain* Juz: 5 kimehakikiwa na Hamdiy ad Dar Madaash Muhammad, Maktaba ya Asiriyah Beirut 2006 kitabu *Maarifatu Swahabah* Uk. 17841 – 1741 Hadith No: 4630

Mwanahadithi na hafidhi kutoka Morocco, ametunga kitabu kinachoitwa: *Fatuhul-Maliki Al-Aliy*, juu ya usahihi wa hadithi ya “*Lango la Jiji la elimu*” kuwa ni Ali (a.s.) (kitabu hicho kimechapishwa na Darul-kutubil- Islamy Beirut)<sup>12</sup>

Humo ametaja hoja za usahihi wa hadithi hii. Ama al-Hakim an-Nisabury yeeye ametaja katika *Mustadrak*:

عن ابن عباس رضي الله عنهما قال: قال رسول الله: أنا مدينة العلم وعلى بابها، فمن  
أراد المدينة فليأت الباب

**“Kutoka kwa Ibnu Abbasi (ra) kwamba amesema: Amese-  
ma Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): Mimi ni Jiji  
la elimu na Ali ni lango lake anayetaka Jiji basi aliendee  
lango.”**

Hadithi hii sanadi yake ni sahihi na (Bukhari na Muslim) hawajaiandika. Abu Swalti ni mkweli na mwaminifu, kwani mimi nimemsikia Abu Abbasi Muhamadi bin Ya'aqub katika Tarikh anasema: Nimemsikia Abbasi bin Muhammad Daury anasema: Nilimuuliza Yahya bin Mu'in kuhusu Abu As Swalti Al-Harawiry akasema: Ni mkweli.

Nikasema: Je siamesimulia juu ya Abu Muawiya kutoka kwa Al-A'amash “Mimi ni Jiji la Elimu.” Akasema amesimulia kwayo Muhamad bin Jafar Al- Faidiy naye ni mkweli, mwaminfu, nimemsikia Abu Nasri Ahmad bin Sahal Al-Faqih Al-Qabaniy Imam wa zama zake huko Bukhary anasema: Nilimsikia Swalih bin Muhammad bin Habib Al-Hafidh anasema: Na aliulizwa kuhusu Abu Swalti Al- Harawiy

<sup>12</sup> Tunatamani Mashia wanunue vitabu vinavyoelezea fadhila za Ahlul bait (as) sifa zao na karama zao.

akasema: Yahya bin Mu'in aliingga na sisi kwa pamoja kwa Abu Swalti, akamsalimia, na alipotoka nilimfuata nikamwambia: Mungu akurehemu unasemaje kuhusu Abu Swalti? Akasema: Ni mkweli. Nikamwambia hakika yeye anapokea hadithi ya Al-A'amash kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Abbas kutoka kwa Nabii (s.a.w.w.): "Mimi ni Jiji la elimu na Ali ni lango lake, mwenye kutaka elimu basi aiendee kupitia lango lake."<sup>13</sup> Akasema amepokea haya yule Faidiy kutoka kwa Abu Muawiya, na Dhahabiy amesema: Bali ni uongo. Na Al-Hakim amesema: Abu Swalti ni mkweli na mwaminifu, na Dhahabiy akasema: Hapana Wallahi si mkweli wala si mwaminifu.<sup>14</sup>

### **Pamoja na kukataa Dhahabiy:**

عن ابن عباس رضي الله عنهم قال: قال رسول الله: أنا مدينة العلم وعلى بابها، فمن  
أراد المدينة فليأت الباب

**"Kutoka kwa Ibnu Abbasi (ra) kwamba amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ( saww): Mimi ni Jiji la elimu na Ali ni lango lake anayetaka Jiji basi aliendee lango."**

Huseini bin Faham amesema: Ametusimlia hiyo Abu Swalti Al-Harawiy kutoka kwa Abu Muawiya. Al-Hakim amesema: Na afahamu mwenye kutaka kunufaika na elimu hii kwamba Husein bin Faham bin Abdul-Rahman ni mkweli, mwaminifu na ni hafidh. Na hadithi hii ina ushahidi kutoka kwenye hadithi ya Sufian Athauriy iliyokuja kwa sanadi sahihi. Na Dhahabiy amesema: Ni ajabu ilioye kwa Al-Hakim na ushujaa wake, anasahihisha haya na mfano wake

<sup>13</sup> Tazama upinzani wao kwa kila aliyepokea fadhila kati ya fadhila za Amirul-Muuminina (as) na ona namna gani shakhisiya hii adhim ilivyodhulumiwa.

<sup>14</sup> al-Hakim an-Nisaburi rejea iliyotangulia Uk. 1743 – 1744 Hadith No: 4637

kati ya yale batili, na huyu Ahmad bin Abdillah bin Yazidi Al-Haraniy ni muongo.

**Jabir bin Abdillah (r.a):**

عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عُثْمَانَ التَّيْمِيِّ قَالَ: سَمِعْتُ جَابِرَ بْنَ عَبْدِ اللَّهِ يَقُولُ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ يَقُولُ: أَنَا مَدِينَةُ الْعِلْمِ وَعَلَيْهَا بَابٌ، فَمَنْ أَرَادَ الْمَدِينَةَ فَلْيَأْتِ بَابَهَا

**Kutoka kwa Abdur Rahman bin Uthman At-Taymiy amesema: Nilimsikia Jabir bin Abdillah anasaema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) anasema: Mimi ni Jiji la elimu na Ali ni lango lake, mwenye kutaka kuliendea basi apitie katika lango lake.”**

**Utti:**

Mwenyezi Mungu ametuamuru kumtii Yeye, Mtume wake (s.a.w.w.) na wenyе mamlaka, Je unadhani ni nani hao wenyе mamlaka? je ni watawala, kama wanavyodai masheikh wa masultan?<sup>15</sup> Kama itasemwa kuwa wenyе mamlaka ni watawala kama wanavyodai masheikh wa masultan ingewajibika kwa watu wa Iraki kumtii Sadam Husein, Mungu amlaani, au kiongozi yejote dhalim. Bila shaka akili iliyo sawa na salama inatuongoza na kututoa kwenye shubuhati na kutufikisha kwenye natija, na natija hii inasema: Ni muhali Mwenyezi Mungu kuniamuru kuwatii watu wasiokuwa maasum, kwa sababu wao wanaweza kutumbukia katika makosa, na hivyo tunapata natija kwamba utii ni kwa Mwenyezi Mungu, Mtume wake na Ahlul-bait

<sup>15</sup> Baadhi ya masheikh wa masultani wanaharamisha kusherehekeea maulidi ya Mtume wakati ambapo wanasherehekeea sherehe za sikukuu za nchi zao na sikukuu za kuzaliwa wafalme na watawala. Wanazingatia maulid ya Mtume ni bidaa ilihali zile sherehe zinazofanywa kwa amri za masultani wao wanaziona kuwa sio bidaa.

(a.s.) ambao Mwenyezi Mungu amewahifadhi kutokana na kuteleza, kukosea na uchafu, yaani kutokana na kila mabaya, hata kusahau na kufanya makuruhu. Na Amirul-Muuminina (a.s.) ni kati ya waliohifadhiwa, na kwa sababu hiyo Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliambatanisha utii wake na utii wa Amirul-Muuminina (a.s.) kama ambavyo inajulikana kwamba kumtii Mtume ni kumtii Mwenyezi Mungu, na riwaya hii inathibitisha hayo:

**عن أبي ذر قال: قال رسول الله لعلي بن أبي طالب: من أطاعني فقد أطاع الله ومن عصاني فقد عصى الله، ومن أطاعك فقد أطاعني ومن عصاك فقد عصاني.**

**“Katoka kwa Abu Dhar (r.a) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kumwambia Ali bin Abi Talib (r.a): Mwenye kunitii amemtii Mwenyezi Mungu, na mwenye kuniasi amemuasi Mwenyezi Mungu, na Mwenye kukutii amenitii mimi na mwenye kukuasi ameniasi mimi.”**

Sanadi ya hadithi hii ni sahihi lakini (Bukhari na Muslim) hawajaiandika.<sup>16</sup>

**Hatawatoa katika uongofu wala hatawaingiza katika upotovu:**

**عن زيد بن أرقم قال: قال رسول الله: من يريد أن يحيي حياتي ويموت موتى ويسكن جنة الخلد التي وعدني ربّي فليتول على بن أبي طالب فإنه لن يخرجكم من هدى ولن يدخلكم في ضلاله.**

**Kutoka kwa Zayd bin Arqam (r.a) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Anayetaka kuishi maisha yangu na kufa kifo changu na kuishi pepo ya milele aliyoniahidi Mola wangu basi na amtawalishe Ali bin Abi**

<sup>16</sup> al-Hakim an-Nisaburi rejea iliyotangulia Uk. 1746 Hadith no: 4641

**Talib, hakika ye ye hatowatoa katika uongofu wala hatowain-giza katika upotovu.”**

Sanadi ya hadithi hii ni sahihi lakini (Bukhari na Muslim) hawajaiandika. Dhahabiy amesema: Itakuwaje sahihi na hali Qasim bin Bashir ni mwenye kuachwa, na sheikh wake ni dhaifu, lafidhi yake ni nyepesi iko karibu mno na uongo.<sup>17</sup>

**Nasema (mwandishi):** Ni ajabu sana jambo la Nasbiy huyu (Dhahabiy). Yeye peke yake ndiye aliyepinga fadhila za Ahlul-bait (a.s.) kana kwamba yeye ndiye peke yake anayefahamu elimu ya hadithi. Ama al-Hakim na Ibnu Al-Maqhazili Ashafiy Al-Khawarizimy, Al-Juwiyiny na wengineo kati ya Maulanaa wa Ahlus-Sunna hawafahamu kitu, yeye tu ndio anayefahamu riwaya na hadithi zote.

**Mjuzi mno wa hukumu kushinda watu wote wa Madina:**

Katika lugha yetu ya Kiarabu kuna zuri na zuri zaidi, bora na bora zaidi, mzuri na mzuri zaidi n.k. Tazama riwaya hii utakuta neno *Aqdhwaa* (mjuzi zaidi wa hukumu):

عن عبد الله قال: كنا نتحدث أن أقضى أهل المدينة على بن أبي طالب

**Kutoka kwa Abdillah amesema: “Tulikuwa tunazungumza kwamba mjuzi wa hukumu kushinda watu wote wa Madina ni Ali bin Abi Talib.”**

Hadithi hii ni sahihi kwa sharti la Masheikh wawili (Bukhari na Muslim) lakini hawajaiandika, na Dhahabiy amenyamaza kimya kuihusu.<sup>18</sup>

<sup>17</sup> al-Hakim an-Nisaburi rejea iliyotangulia Uk. 1746 Hadith no: 4642

<sup>18</sup> al-Hakim an-Nisaburi rejea iliyotangulia Uk. 1757 Hadith no: 4656.

### **Usalama wa dini yake:**

Shaitani hampati Amirul-Muuminina (a.s.) kama vile anavyowapata baadhi, Imam Ali ni maasum kutokana na makosa, hawezi kukosea wala kuteleza, hivyo yeye ni salama katika dini yake kama ilivyokuja katika hadith, na hii ni moja kati ya hizo:

عن ابن عباس رضي الله عنهم قال: قال النبي لطفي: أما أنك ستقى بعدي جهدا. قال:  
في سلامة من ديني؟ قال: في سلامة من دينك.

"Kutoka kwa Ibnu Abbas (r.a) amesema: Nabii (s.a.w.w.) alisema kumwambia Ali (a.s.): «Ama hakika wewe utapata taabu kubwa baada yangu.» Akasema: Je, nitakuwa salama katika dini yangu? Akasema: «Utakuwa salama katika dini yako.»"

Hadith hii ni sahihi kwa sharti la Masheikh wawili (Bukhari na Muslim) lakini hawajaiandika. Dhahabiy amesema: Kwa sharti la Bukhariy na Muslim ni sahihi.<sup>19</sup>

### **Vizito viwili:**

Je, unaitakidi kwamba Mwenyezi Mungu anaweza kumkabidhi uongozi wa waja Wake yule mwenye kukosea? Bila shaka jawabu litakuwa ni hapana. Kwani hii ni kinyume na uadilifu wa kiungu kama ambavyo historia ya kila Nabii imetuthibitishia, kwamba kila Nabii alikuwa na Wasii Maasum, kwa mfano wasii wa Adam ni mtoto wake Shith, wasii wa Ibrahim ni mtoto wake Ismail, wasii wa Ya'aqub ni mtoto wake Yusufu, wasii wa Daud ni mtoto wake Suleimani, wasii wa Musa ni ndugu yake Haruna na wasii wa Nabii wetu

---

<sup>19</sup> al-Hakim an-Nisaburi rejea iliyo tangulia Ukt. 1759 Hadith no: 4677

(s.a.w.w.) ni Amirul-Muuminina (a.s). Yeye ndio Khalifa wa kisheria na ndio Mwenye mamlaka. Riwaya zinathibitisha umaasum wa Imam Ali (a.s) sambamba na kiakili, na Hadithi ya vizito viwili ni ushahidi mzuri juu ya umaasum wa Amirul – Muuminina (a.s),<sup>20</sup> kwa sababu humo kuna mafungamano na Kitabu ambacho hakipatwi na batili kutoka katika Torati wala kutoka katika Injili. Natija hiyo tunaipata kutoka katika kauli yeke (s.a.w.w.): “Havitotengana hadi vitakaponijia katika hodhi yangu.”

عن زيد بن أرقم قال: قال رسول الله: إني تارك فيكم الثقلين كتاب الله وأهل بيتي، وإنهما لن يتفرقان حتى يردا على الحوض.

Kutoka kwa Zayd bin Arqam (r.a) amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Hakika mimi ninawaachieni vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahali baiti wangu, hakika hivyo viwili havitotengana hadi vitakaponijia katika hodhi.”

Sanadi ya hadith hii ni sahihi kwa sharti la masheikh wawili (Bukhari na Muslim) lakini hawa jaiandika. Dhahabiy amesema kwa sharti la Bukhari na Muslim ni sahihi.<sup>21</sup>

### Rai ya Ibnu Taimiya:

Ibnu Taimiya alikuwa anaona kwamba Amirul-Muuminina (a.s) alikuwa anajua hukumu zaidi kushinda masahaba wengine wote. Anasema katika kitabu *Istiqamah*: “Tunajua kwamba Ali (a.s) alikuwa anajua hukumu zaidi kushinda wengine kutohana na alivyoyafahamu hayo, pamoja na

<sup>20</sup> Tumetaja katika kitabu” *Baina Twalal Husein* sura kamilii juu ya umaasum, na kuna vitabu na utafiti mwingi juu ya umaasumu wa manabii na umaasum wa Ahlul bait, tunataraji kwamba watapata raghaba ya kukinunua.

<sup>21</sup> al-Hakim an-Nisaburi Uk. 1770 Hadith no: 4711.

kwamba kusikiliza maelezo kulikuwa na ushirikiano baina yake na asiye kuwa yeye.”<sup>22</sup>

Hivyo inatubainikia sisi na wale wafuasi wa Ibnu Taimiya kwamba Imam Ali (a.s) ni mtu bora katika umma huu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), hiyo ni kwa sababu Ibnu Taimiya amenukuu katika kitabu chake *Al-Imanul ausati* hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kwa maana hii. Amesema (s.a.w.w.): “Mbora wenu ni yule ajuaye zaidi hukumu.”

**Nasema:** Hakika ni juu ya Ahlus Sunna kutazama upya mas’ala mengi, na muhimu zaidi kati ya hayo ni ukhalifa na umaasum, kwani kiongozi au khalifa wa kisharia ni wajibu awe maasum ili asiwapoteze watu njia ya sawa. Ibnu Taimiya ananukuu katika kitabu chake alichomjibu Kadhi wa Kimalikia kiitwacho *Aradu Alal-Akhinaaiy*: “Katika Sahihaini kuna riwaya kutoka kwa Abdillah bin Amru kutoka kwa Nabii (s.a.w.w.) kwamba hakika amesema: ‘Hakika Mwenyezi Mungu hahifadhi elimu kwa kuitoa kwa watu, bali huihifadhi kwa kuwashifadhi Maulamaa, kama mwanachuoni hatabakia basi watu watawafanya majahili kuwa viongozi, hivyo wataulizwa na watatoa fatwa bila ya elimu, hapo watapotea na kupoteza! Na ilivyo katika riwaya ya Bukhari ni ‘watatoa fatwa kwa rai zao.’”<sup>23</sup>

Riwaya hii inatubainishia umuhimu wa elimu na khalifa wa kisheria wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ni wajibu awe mwenye elimu na maasum ili asiwapotoshe watu katika njia ya sawa, na katika kitabu hiki tutapitia baadhi ya visa ambavyo humo haki inadhihirika wazi pale Khalifa wa

<sup>22</sup> *Al-Istiqaamah* kimehakikiwa na Ahmad Jaad. Darul Hadith Cairo 2005 Uk. 16.

<sup>23</sup> *Aradu Alal-Akhinaaiy*, kimehakikiwa na Adaniy bin Aal Zahawiy – Al-Maktabatu Al-Asiriya Beirut chapa ya kwanza 2002 Uk. 17

kisheria wa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliyeporwa haki yake, Ali bin Abi Talib (a.s), anapowasahihisha Makhalifa makosa mengi ambayo walitumbukia humo. Isipokuwa Mwenyezi Mungu (swt) alitaka kuwabainishia watu haki ya Imam Ali (a.s) katika ukhalifa na haki yake kwa asiyekuwa yeeye, na hiyo ni kupitia kitendo cha Imam Ali (a.s) kuingilia kati na kuwaokoa baadhi ya wale ambao khalifa alikaribia kupitisha hukumu ya adhabu juu yao. Hivyo kuamini umaasum ni wajibu kwa sababu umaasum wa khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt) unamaanisha kwamba hukumu za khalifa huyu ni hukumu za Mwenyezi Mungu, zinanufaisha watu na wala hazimdhuru yeyote.

### **Jiji la elimu:**

قال رسول الله: أنا مدينة العلم وعلى بابها، فمن أراد المدينة فليأت الباب

**Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): "Mimi ni Jiji la elimu na Ali ni lango lake, anayetaka elimu basi aliendee lango."**<sup>24</sup>

### **Elimu ya Adam:**

قال رسول الله: من أراد أن ينظر إلى آدم في علمه وإلى نوح في فهمه وإلى يحيى بن زكريا في زهده، وإلى موسى بن عمران في بطشه فلينظر إلى علي بن أبي طالب.

**Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mwenye kutaka kumtazama Adamu katika elimu yake, Nuh katika fahamu yake, Yahya bin Zakariya katika zuhudi yake, Musa bin Iman katika ushujaa wake basi amtazame Ali bin Abi Talib."**<sup>25</sup>

<sup>24</sup> *Maqtalul-Imami Husein* Juz. 1, Daru Anuwaril Huda, Qum chapa ya kwanza 1418 Sura ya nne Uk. 76 - 92 , hadith no: 24 .

<sup>25</sup> Rejea iliyotangulia Uk. 76 -77 hadith no: 25

### Kama nikiwekewa mto:

Kutoka kwa Abu Al-Bakhitariy amesema: Nilimuona Ali akipanda mimbari huko Kufa, akiwa na ngao ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, akiwa ameshikilia upanga wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ( s.a.w.w.), amevaa kilemba cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na katika kidole chake kuna pete ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), akakaa juu ya mimbari na akasema:

سلوني قبل أن تغدوني، فإنما بين الجوانح علم جم، هذا سبط العلم، هذا لاعب رسول الله، هذا ما زقني رسول الله زقاً من غير وحي أوحى إلي، فوالله لو ثبتت لي الوسادة وجلست عليها لأفتتح لأهل التوراة بتوراتهم، ولأهل الإنجيل بإنجيلهم، حتى ينطق الله التوراة والإنجيل فيقولا: صدق علي قد أفتاتكم بما أنزل فينا وأنتم تتلون الكتاب فلا تعقولون.

**"Niulizeni kabla hamjanikosa hakika pembezoni mwangu kuna elimu nyingi mno, huu ni mkoba wa elimu, huu ni ute wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, haya ni ambayo amenifundisha Mtume wa Mwenyezi Mungu pasina ya kuwa ni wahyi uliofanuliwa kwangu, wallahi kama nitatandikiwa mto na nikakaa juu yake ningetoa fatwa kwa watu wa Torati kwa Torati yao na watu wa Injili kwa injili yao, na hadi Mwenyezi Mungu angeitamkisha Torati na Injili na kusema: Ali amesema kweli, amewatolea fatwa kwa yale yaliyoteremshwa kwetu, na nyinyi mnasoma Kitabu je, hamna akili?"<sup>26</sup>**

---

<sup>26</sup> Maqtalul-Imami Husein Juz.1, Daru Anuwariil Hudaa, Qum chapa ya kwanza 1418 Sura ya saba Uk. 91 - 92

### Wapi imeshuka?:

عَنْ عَلِيٍّ قَالَ: وَاللَّهِ مَا نَزَّلَتْ آيَةً إِلَّا وَقَدْ عَلِمْتُ فِيمَا أَنْزَلْتَ وَأَنِّي أَنْزَلْتُ وَأَنَّ رَبِّي وَهُبَّ لِي قُلْبًا عَقُولًا وَلِسَانًا سُؤُولًا.

Kutoka kwa Ali amesema: "Haijashuka Aya ila nimesha-jua kwa nini imeshuka na wapi imeshuka, na hakika Mola wangu amenipa moyo wenyewe akili na ulimi wenyewe kuuliza."

### Usiku au mchana:

قَالَ عَلِيٌّ بْنُ أَبِي طَالِبٍ: سَلَوْنِي عَنْ كِتَابِ اللَّهِ فَإِنَّهُ لَيْسَ مِنْ آيَةٍ إِلَّا وَقَدْ عَرَفْتُ أَبْلِيلَ نَزَّلَتْ أَمْ بِنَهَارٍ أَمْ فِي سَهْلٍ أَمْ فِي جَبَلٍ.

Ali bin Abi Talib (a.s) amesema: "Niulizeni kuhusu Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwani hakuna Aya isipoku-wa najua ilishuka mchana au usiku, kwenye tambarare au mlimani."<sup>27</sup>

### Simjui:

Kutoka kwa Atwai, aliulizwa je katika masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kulikuwa na yeoyote aliyekuwa mjuzi zaidi kushinda Ali? Akasema simjui. Ameiandika Al-Qala'iy.<sup>28</sup>

عَنْ أَبْنَى مُسْعُودٍ قَالَ: أَعْلَمُ أَهْلَ الْمَدِينَةِ بِالْفَرَائِصِ عَلِيٌّ بْنُ أَبِي طَالِبٍ.

Na kutoka kwa Ibnu Mas'udi (r.a) amesema: "Mjuzi zaidi wa faraidhi (mirathi) kushinda watu wote wa Madina ni Ali bin Abi Talib."

<sup>27</sup> Rejea iliyotangulia Uk. 95

<sup>28</sup> Riyadhus-Salihin-Nadhwara Fi Manaqib al-Asharatil-Mubashariyna bil-Jannah, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uk. 141 .

Na kuna nyingine mfano wa hiyo kutoka kwa Mughira, ameipokea Al-Qala'iy.<sup>29</sup>

### Kinywa chake:

عن ابن عباس رضي الله عنهم أنه قال: والله لقد أعطى تسعة عشر من أهل العلم، وأيم الله لقد شاركتم في العشر العاشر.

**Kutoka kwa Ibnu Abbas (r.a) amesema: "Wallahi ali pe-  
wa sehemu tisa kati ya sehemu kumi (9/10) na Wallahi  
anashirikiana nanyi katika sehemu iliyobakia (1/ 10)".**

**Ameiandika Abu Umar.**

Na kutoka kwake (Ibnu Abbas), watu walimuuliza wakasema Ali alikuwa ni mtu wa aina gani? Akasema:

كان ممتنناً جوفه حكماً وعلمًا وبأساً ونجدة مع قرابته من رسول الله.

"Alikuwa amejaa hekima, elimu, ushujaa na msaada, pamo-  
ja na kwamba alikuwa karibu mno na Mtume wa Mwenyezi  
Mungu (s.a.w.w.)." Ameiandika Ahmadi katika kitabu  
Al-Manaqib.<sup>30</sup>

<sup>29</sup> Rejea iliyotangulia

<sup>30</sup> Riyadhus-Salihin-Nadhwara Fiyy Manaqib al-Asharatil-Mubashariyina bil-Jannah, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uk. 141 .

## MLANGO WA PILI

### KATI YA AMIRUL-MUUMININA (A.S.) NA ABU BAKR

وعلموا أن لي شيطاناً يعتريني أحياناً، فإذا رأيتمني غضب فاجتنبني.

"Na jueni kuwa mimi nina shetani ananijia baadhi ya nyakati, mnaponiona nimekasirika basi niepukeni." Hobu ya Abu Bakr.<sup>31</sup>

**Yuko wapi aliye mfano wako ewe Abul-Hassan:**

Kutoka kwa Al-Harith Al-Awar mshika bendera ya Ali bin Abi Talib amesema: Imetufikia habari kwamba Nabii (s.a.w.w.) alikuwa katika kundi la masahaba zake akasema: "Je, niwaonyeshe Adam katika elimu yake, Nuh katika fahamu yake na Ibrahim katika hekima yake?" Haukupita muda akatokea Ali. Abu Bakri akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mtu huyu amelingana na Manabii watatu, pongezi pongezi kwa mtu huyu, ni nani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Nabii akasema: "Je humfahamu ewe Abu Bakr?" Akasema Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanajua. Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: "Ni Abul-Hasan Ali bin Abi Talib." Abu Bakr akasema: Pongezi pongezi kwa Abul-Hasan Ali bin Abi Talib, na yuko wapi aliye mfano wako ewe Abul-Hasan.<sup>32</sup>

<sup>31</sup> *Al-Imamah Wassiasah*, Darul-Kutubi al-iliyyah Beirut chapa ya pili 2006 Uk.19

<sup>32</sup> *Al-Manaqib*, Muasasatul balagha Beirut chapa ya 2005 Sura ya saba Uk. 90-91.

## **Mjuzi zaidi kushinda wengine katika kutoa wasifu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.):**

Kutoka kwa Ibnu Umar amesema kwamba, Mayahudi walikuja kwa Abu Bakr wakamwambia tupe wasifu wa Swahiba yako. Akasema: "Enyi Mayahudi nilikuwa pamoja naye pangoni kama vidole vyangu hivi na nilishapanda naye mlima wa Hirai na kidole changu kidogo kiko katika kidole chake, lakini kutoa wasifu wake (s.a.w.w.) ni kazi ngumu sana, lakini huyu hapa Ali bin Abi Talib." Wakamwendea Ali wakamwambia: Ewe Abul-Hasan tupe wasifu wa mtoto wa Ami yako. Akasema:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwa mrefu sana wala sio mfupi sana alikuwa wa kati, mweupe wa rangi mwenye kumili kwenye wekundu, mwenye nywele ngumu, sio za kipilipili, nywele zake zinaangukia kwenye mabega yake, mpana wa uso, wenyе macho makubwa, mwenye nyusi nyeusi, mwenye mwaya, mwenye pua yenyе kuchongoka kana kwamba ni mkono wa birika la fedha, ana nywele kutoka kwenye koo lake hadi kwenye kitovu chake kana kwamba ni fimbo ya miski nyeusi, hapakuwepo katika mwili wake wala katika kifua chake nywele isipokuwa hizi, na alikuwa na viganja madhubuti na nyayo ngumu na anapotembea ni kana kwamba anateremka kutoka kwenye jabali, anapogeuka anageuka mzima mzima kwa mwili wake wote, anaposimama anawaenea watu, na anapokaa anakuwa katikati ya watu.

Anapoongea watu wananyamaza, na anapohutubia anawaliza watu, alikuwa ni mpole mno kati ya watu, alikuwa ni kama baba mwenye huruma kwa yatima, mkarimu kwa wajane, shujaa na mkarimu, mwenye uso wa mvuto, vazi lake ni joho, chakula chake ni mkate wa shairi, mboga yake

ni maziwa, na mto wake ulifumwa kwa majani ya mtende, kitanda chake ni cha kamba, alikuwa na vilemba viwili kimoja kinaitwa *As-Sahab* na kingine kinaitwa *Al-Aqab*, upanga wake ni *Dhul-Fiqr*, bendera yake ni *Al- Gharau*, punda wake ni *Ya'afur*, farasi wake ni *Murtajiz*, kondoo wake ni *Barakat* na fimbo yake ni *Al-Mamshuq* na bendera ya kikosi chake ni *Alhamdi*, alikuwa anapanda ngamia, anaweka viraka nguo zake na anashona viatu vyake.”<sup>33</sup>

---

<sup>33</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fiyy Manaqib al- Asharatiil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uk.143.

## MLANGO WA TATU

### **KATI YA AMIRUL-MUUMININA (A.S.) NA UMAR BIN AL-KHATTAB**

#### **Umar hajui:**

Katika riwaya hii yenye sanadi sahihi ambayo ameipokea Imam Ahmad bin Hanbali katika kitabu *Fadhalus-Sahaba* tunapata maelezo ya kukiri kwa Khalifa Umar kwamba alikosea katika hukumu. Riwaya inasema:

Kutoka kwa Abu Dhabiyan Al-Janbiy, hakika Umar bin Al-Khattab aliletewa mwanamke aliyezini akasema: "Apigwe mawe." Wakawa wanakwenda kumpiga mawe, wakiwa njiani wakakutana na Ali akawauliza: "Ana nini huyu?" Wakasema amezini na Umar ameamuru apigwe mawe. Ali akamchukua toka kwao na wakarejea kwa Umar, Akawauliza nini kimewarejesha? Wakasema Ali ameturejesha. Akasema Ali hakufanya hivi isipokuwa kuna jambo amelijua, akatuma Ali aitwe, akaja naye akiwa amekasirika. Umar akasema: "Una nini umewarejesha hawa?" Ali akasema: "Hujamsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: Watu watatu wamesamehewa: Aliyelala hadi aamke, mtoto mdogo hadi abaleghe na kichaa hadi akili yake irejee?" Akasema ndio nimesikia. Ali akasema: "Huyu ni kichaa wa Bani Fulan, na huenda ameingiliwa naye akiwa ni kichaa." Umar akasema, sijui. Ali naye akasema na mimi pia sijui, basi hakupigwa mawe. Katika maelezo ya pembezoni: Sanadi yake ni sahihi.<sup>34</sup>

<sup>34</sup> Ahmad bin Hanbal: *Fadhalus-Sahabah*. Kimehakikiwa na Wasiyullah bin Muhamda Abbas daru Ibnu Al- Jauziy – Al-mamlakatul Arabiya Saudiyah, chapa ya tatu 1426A.H. Uk. 880 –881 hadith no: 1209 .

### **Alitaka kumpiga mawe:**

Kutoka kwa Amru kutoka kwa Hasani, hakika Umar bin Al- Khattab aliletewa mwanamke kichaa mjamzito ameshazini akataka kumpiga mawe, Ali akamwambia: "Je, hujasikia aliyyoyasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)?" Akasema: Na amesema nini? Ali akasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: Kalamu imesimamishwa kwa watu watu: Kichaa hadi apone, mtoto hadi abalaghe na aliylala hadi aamke." Basi akamwachia.<sup>35</sup>

### **Kama sio Ali Umar angeangamia:**

Amenisimulia Zayd bin Ali kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake Ali bin Abi Talib kwamba amesema: Wakati wa utawala wa Umar aliletwa mwanamke mjamzito, Umar akamuuliza juu ya hilo akakiri kufanya uchafu, Umar akaamua apigwe mawe. Wakiwa njiani wakakutana na Ali akawauliza, mwanamke huyu ana jambo gani? Wakasema Umar ameamuru apigwe mawe, Ali akamrejesha akamuuliza Umar: "Umeamuru apigwe mawe?" Akasema ndio, amekiri mbele yangu kufanya uchafu. Ali akasema: "Haya ni mamlaka yako juu yake. Ni yapi mamlaka yako kwa aliye tumboni mwake?" Kisha Ali akamwambia: "Pengine umemkemea au umemtisha!" Akasema ndiyo ilikuwa hivyo. Ali akasema: "Je hujamsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) anasema: 'Hakuna adhabu kwa aliyekiri baada ya balaa.' Kwamba aliyefungwa pingu, mahabusu au aliyetishwa kukiri kwake hakuna maana." Umar akamwachia huru

<sup>35</sup> *Al-Manaqib*, Muasasatul balagha Beirut chapa ya 2005 Sura ya saba Uk. 83.

kisha akasema: "Wanawake wameshindwa kuzaa mfano wa Ali bin Abi Talib, kama sio Ali Umar angeangamia."<sup>36</sup>

### **Ali ndio mjuzi wetu zaidi wa hukumu:**

Kutoka kwa Ibnu Abbas amesema: Alituhutubia Umar akasema: "Ali ndio Mjuzi wetu zaidi wa hukumu na Ubayya ndio msomaji wetu."<sup>37</sup>

### **Rejesheni kauli ya Umar kwa Ali:**

Kutoka kwa Amir kutoka kwa Masuruq, amesema: Umar aliletewa mwanamke aliyeolewa katika eda yake, akawatenganisha na mahari yake akayapeleka katika Baitul-Mali. Akasema: "Si ruhusa mahari, rejesheni ndoa yake." Na akasema: "Hawataunganika tena abadani." Ashiath ameongezea: Habari ikamfikia Ali, yeye akasema: "Hata kama hawakujua Sunna lakini ana mahari kwa kuingiliwa kwake na wanatenganishwa. Eda yake ikimalizika yeye atakuwa mposaji kati ya waposaji." Umar akahutubia watu akasema:

رَدُوا الْجَهَلَاتِ إِلَى السَّنَةِ وَرَدُوا قَوْلَ عَمَرٍ إِلَى عَلَيِّ

**"Warejesheni wasiojua kwenye Sunna, na rejesheni kauli ya Umar kwa Ali."**

### **Mwenye maghafir:**

Kutoka kwa Ibnu Siriyn amesema: Hakika Umar aliuliza watu: "Anayemilikiwa anaolewa mara ngapi?" Na

<sup>36</sup> *Al-Manaqib*, Muasasatul balagha Beirut chapa ya 2005 Sura ya saba Uk. 83 - 84.

<sup>37</sup> *Al-Manaqib*, Muasasatul balagha Beirut chapa ya 2005 Sura ya saba Uk. 93

akamwambia Ali nakukusudia wewe ewe mwenye *maqhfifry* (nguo aliyokuwa amejitanda), Ali akasema: "mara mbili."

### **Dua ya Umar bin al-Khattab:**

Kutoka kwa Said bin Al-Musayab amesema: Nilimsikia Umar, anasema: "Eee Mwenyezi Mungu! usinibakishe katika tatizo ambalo Ali bin Abi Talib atakuwa hayupo hai."<sup>38</sup>

### **Anamfundisha Umar hukumu:**

Kutoka kwa Abdillah bin Abbas amesema: Mtu alimshitaki Ali bin Abi Talib kwa Umar bin al-Khattab, na Ali alikuwa amekaa katika majlis ya Umar bin al-Khattab, Umar akamgeukia Ali na kusema: "Ewe Abul-Hasan!" akasema mwenye kuunga mkono: "Simama ukae na hasimu wako." Ali akasimama na akakaa na hasimu wake wakatazamana. Yule mtu akaondoka na Ali akarejea katika sehemu yake ya mwanzo, Umari akagundua mabadiliko katika uso wake, akamwambia: "Ewe Abul-Hasan vipi mbona naona mabadiliko katika uso wako? Je umechukia yaliyotokea?" Akasema. "Ndio." Umar akasema, na kwa nini imekuwa hivyo? Ali akasema: "Kwa sababu umeniita kwa heshima Abul-Hasan mbele ya hasimu wangu. Je hujasema: Simama ewe Abul-Hasan kaa na hasimu wako?" Umar akashika kichwa cha Ali akabusu paji la uso wake kisha akasema: "Naapa kwa baba yangu, kupitia kwenu nyinyi Mwenyezi Mungu ametuongoa na kupitia kwenu ametutoa kutoka kwenye giza kwenda kwenye nuru."

### **Ushujaa:**

Kutoka kwa Muhammad bin Khalid Adhwabiy amesema: Umar bin al-Khattab aliwahutubia watu akasema: "Kama

<sup>38</sup> *Al-Manaqib*, Muasasatul balaghha Beirut chapa ya 2005 Sura ya saba Uk. 97

nitawatoa katika yale mnayoyajua kwenda katika yale mnayoyapinga mtafanyaje?" Muhammad akasema: Wakanyamaza. Akasema hayo mara tatu, ndipo Ali akasimama akasema: "Ewe Umar! Tutakutaka utubu, ikiwa utatubu tutakukubalia." Umar akasema: "Na kama sitatubu?" Ali akasema: "Basi tutakata kichwa chako." Umar akasema: "Alhamdulilahi Ambaye amejaalia katika umma huu mtu ambaye tunapopindisha mambo anasitisha matakwa yetu."

**Nasema:** Hii ni dalili kubwa kabisa kutoka katika vitabu vyao kwamba Imam Ali (a.s.) ndiye anayeamrisha mema na kukataza maovu, na wala haogopi watawala, tazama ushujaa wake katika kumjibu Umar pamoja na kunyamaza masahaba waliobakia, kama ambavyo riwaya hii inaonyesha juu ya umaasum wa Imam Ali (a.s.) na juu ya ujuzi wake, kwa sababu yeye ndio pekee ambaye aliyeweza kusahihisha makosa ya Khalifa.

### **Malipo ya wale waliofasiri Aya kwa rai zao:**

Kutoka kwa Abdur Rahmani amesema: Watu walikunyuwa pombe huko Sham katika ugavana wa Yazid bin Abi Sufian katika zama za Umar. Yazidi akawaambia Je, mmekunyuwa pombe? Wakasema ndio tumekunyuwa nayo ni halali kwetu akasema: Je, Mungu si anasema: "**Enyi mlolioamini hakika pombe na kamari**" hadi kwenye kauli yake "**na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake**" hadi akamalizia Aya. Wakasema: Soma Aya inayofuatia. Akasoma "**wala hakuna ubaya kwa wale walioamini na kufunya amali njema kwa yale waliyokunyuwa**"<sup>39</sup> hadi kwenye kauli yake; "**Na Mwenyezi Mungu anawapenda watu wema.**" Hivyo sisi ni kati ya wale walioamini na kufanya vizuri.

<sup>39</sup> Suratul- Maida: 90-93

Yazid akaandika kuhusu jambo lao kwa Umar, Umar akamwandikia: "Barua yangu itakapokufikia usiku kusikuche hadi uwatume kwangu na ikikuflikia mchana basi lisichwe hadi uwalete kwangu." Akawapeleka kwake, walipowasili kwa Umar akawaauliza kama alivyowauliza Yazidi, na wakamjibu kama walivyomjibu Yazidi, akataka ushauri kutoka kwa masahaba wa Nabii lakini wao wakarejesha ushauri kwake mwenyewe. Ali alikuwa hadhiri hapo katika hali ya ukimya, ndipo Umar akasema unasemaje Ewe Abul-Hasan? Amirul-Muumini (a.s.) akasema: "Hakika wao ni watu waliomzulia uongo Mwenyezi Mungu na wamehalalisha aliyoharamisha Mwenyezi Mungu, naona watubishwe, na kama watang'ang'ania na kudai kuwa pombe ni halali watakatwa shingo zao. Na kama watarejea utawapiga mijeledi themanini kwa kumsingizia Mwenyezi Mungu Mtukufu." Wakasema akawaita wakasikiliza maneno ya Ali. Akasema mnasemaje? Wakasema: Tunaomba maghfira na kutubia kwa Mwenyezi Mungu na tunashuhudia kwamba pombe ni haramu. Basi akawapiga mijeledi themanini.

### **Dua ya Umar bin al-Khattab:**

Kutoka kwa Yahya bin Aqiyl amesema: Umar bin al-Khattab alikuwa anamwambia Ali bin Abi Talib kutokana na yale aliyokuwa anamuuliza na kumtatulia "Mwenyezi Mungu asinibakishe baada yako ewe Ali."<sup>40</sup>

### **Muulize Ali:**

Kutoka kwa Udhainah al-Abadiy anasema: Nilimwendea Umar nikamuuliza wapi nitahirimia Umra? Akasema:

<sup>40</sup> Al-Khawarizimy, rejea iliyotangulia Uk. 100

“Mwendee Ali umuulize.” Ameipokea Abu Amru na Ibnu Saman katika *Al-Muwafaqah*.<sup>41</sup>

### **Aliyelazimishwa (Aliyedharurika):**

Kutoka kwa Abdur-Rahmani Asalmiy amesema: Umar aliletewa mwanamke aliyepwata na kiu akapitia kwa mchungaji akaomba maji, naye akakataa kumpa maji hadi akubali kuzini naye, basi akafanya hivyo. Umar akaomba ushauri kwa watu katika kumpiga mawe. Ali akamwambia: “Huyu amelazimika kufanya, hivyo mwachie.” Basi akawachia.<sup>42</sup>

### **Hila:**

Kutoka kwa Hanashi bin Al-Mu’utamir kwamba watu wawili walimwendea mwanamke wa kikuraishi, wakaweka dinari laki moja na wakasema usimpe mmoja wetu bila ya kuwepo sahiba yake, hadi tuwepo sote. Wakakaa mwaka kisha mmoja wao akaja kwake na akasema: “Hakika sahiba yangu amefariki hivyo nipe zile dinari,” akakataa. Lakini jamaa zake wakamuwia uzito na hawakuacha kuwa kwake hadi akampa hizi dinari. Kisha akakaa mwaka, na ndipo akaja mwingine akasema: “Nipe zile dinari.” Akasema hakika sahiba yako alinijia na akadai kwamba wewe umefariki hivyo nikampa. Wakashitakiana kwa Umar, naye akataka kumhukumu. Pia imepokewa kwamba ye ye alimwambia sioni ila wewe ni mwenye dhamana. Akasema nakumomba usituhukumu bali tipeleke kwa Ali bin Abi Talib. Akampeleka kwa Ali na Ali akatambua kwamba wao walimfanyia hila. Ali akasema: “Je simlisema usimpe mmoja wetu bila ya kuwepo sahiba yake?”

<sup>41</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fi Manaqib al-Asharatil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 U.K.142.

<sup>42</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fi Manaqib al-Asharatil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 U.K.144.

Wakasema ndio. Akasema: "Hakika mali yako ipo kwetu nenda ukamlete sahiba yako ili tuwape."<sup>43</sup>

### **Kugawa mali:**

Kutoka kwa Musa bin Talha amesema kwamba, ilikusanyika kwake Umar mali akaigawa, kikabaki kwake kiasi cha fedha naye akawashauri wafuasi wake katika ziada hiyo. Wakasema tunaona uitunze kama utahitaji chochote basi itakuwa kwako – na Ali alikuwa yuko kimya mionganoni mwao - Umar akasema una nini huongei ewe Ali? Akasema: "Watu wameshakushauri." Akasema, nawe pia toa ushauri. Ali akasema: "Mimi naona uigawe." Basi akafanya hivyo.<sup>44</sup>

### **Audhubillahi:**

Kutoka kwa Abu Said Al-Khudury amesema kwamba alimsikia Umar anamwambia Ali wakati ameshamuuliza juu ya jambo na akamjibu: "Audhubillahi kuishi katika kaum ambayo hayupo humo Abu Hasan."<sup>45</sup>

---

<sup>43</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fi Manaqib al-Asharatil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uk. 145 - 146 .

<sup>44</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fi Manaqib al-Asharatil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uk. 146 .

<sup>45</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fi Manaqib al-Asharatil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uk. 146.

## MLANGO WA NNE

---

### **BAINA YA AMIRUL-MUUMININA (A.S.) NA UTHMAN BIN AFFAN**

---

**Mwanamke wa Kianswari:**

Kuhusu Muhammad bin Yahya bin Munqidh: Chini ya himaya yake kulikuwa na wanawake wawili, mmoja wa Kihashimiya na mwingine wa Kianswari, akamtaliki wa Kianswari, na kisha mume akafariki mwanzo wa mwaka. Mwanamke akasema: "Eda yangu haijaisha." Wakashitakiana kwa Uthman, akasema: "Sina elimu ya hili." Wakaenda kwa Ali, yeye akasema: "Utaapa kwenye mimbari ya Nabii (s.a.w.w.) kwamba hujapata hedhi kwa muda wa miezi mitatu na utapata mirathi." Akaapa, basi akashirikishwa katika mirathi. Ameipokea Ibnu Harbu at-Twaiy.<sup>46</sup>

**Katika Mut'a:**

Amepokea Abu Ya'aliy Al-Muuswily katika *Musnadi* yake ambayo Al-Hafidh Ismail bin Muhammad bin Al-Fadhli At-Tamimi amesema: Nimesoma *Musnad* kama vile *Musnad Al-'Adaniy*, *Musnad Ahmad bin Muniy'i* nayo ni kama mito, na *Musnad Abi Ya'aliy* ni kama bahari yenyе kukusanya mito.

Na Riwaya ni hii: Ametusimulia Ubaidullah amesema: Ametusimulia Ghandar, amesema: Ametusimulia Sha'abah kutoka kwa Amru bin Murrah, kutoka kwa Said bin Al-

<sup>46</sup> *Riyadhus-Salihin-Nadhwara Fiyy Manaqib al-Asharatil-Mubashariyyah bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988, Uk.146.

Musayab kwamba amesema: Walikutana Ali na Uthman, Uthman alikuwa anakataza Mut'a au Umra. Ali akasema: "Unataka nini katika jambo alilolifanya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), unalikataza?" Uthman akasema: "Tuache halikuhusu." Ali akasema: "Siwezi kukuacha." Ali Alipoona hivyo akahirimia kwa vyote pamoja (Mut'a na Umra). Katika maelezo ya pembezoni: Sanadi yake ni sahihi.<sup>47</sup>

**Nasema:** Riwaya hii inaonyesha upeo wa elimu ya Amirul-Muuminina (a.s.) katika Sunna tukufu, tofauti na asiyekuwa yeeye kati ya watu.

---

<sup>47</sup> *Musnad Abi Yaaliy Al-Muuswiliy*. Kimehakikiwa na Husein Saliym Asad, chapa ya Darul-Maamun lil-Iturath Damascus chapa ya pili 1989 U<sup>k</sup>. 284 hadith No: 82 ( 342)

## MLANGO WA TANO

### BAINA YA AMIRUL-MUUMININA (A.S.) NA MU'AWIYA

#### **Mu'awiya:**

Kutoka kwa Abu Hazim amesema: Alikuja mtu kwa Mu'awiya akamuuliza mas'ala. Akasema kamuulize Ali bin Abi Talib yeye ni mjuzi zaidi. Muulizaji akasema: "Ewe Amirul- Muuminina jibu lako linapendeza zaidi kuliko jibu la Ali." Mu'awiya akasema: "Ni mabaya uliyoyasema, umemchukia mtu ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa anamfundisha elimu na ameshasema juu yake: Daraja lako kwangu ni sawa na daraja la Harun kwa Musa ila hakuna Nabii baada yangu. Na Umar alikuwa anapotatizwa na jambo hulichukua kutoka kwa Ali." Ameiandika Ahmad katika kitabu *Al-Manaqib*.<sup>48</sup>

**Nasema:** Pamoja na kutambua kwake hilo kwa nini Mu'awiya alimpiga vita Ali? Bila shaka ni kwa sababu dunia ina thamani kubwa mno kwake, wakati ambapo Amirul-Muuminina yeye huinunua Akhera yake na huiuza dunia yake.

#### **Kiambatanisho:**

Tunataja beti za Swahib bin Ibad alizotaja Al-Khawarizimiy katika kitabu *al-Manaqib*, amesema: Swahib amesema:

---

<sup>48</sup> *Riyadhun-Nadhwara Fiy Manaqib al-Asharatiil-Mubashariyna bil-Jannah*, chapa ya Daru Naduwat al-Jadiyd Beirut chapa ya kwanza 1988 Uki. 142-143

**حب النبي وأهل البيت معتمدى إذا الخطوب أساءت رأيها فيها**

**“Kumpenda Nabii na Ahlul-bait ni tegemeo langu, hata kama watu watakuwa na maoni mabaya dhidi yetu.**

**أبي بن عم رسول الله أفضل من ساد الأنام وساس الهاشميين**

**“Ni yupi mtoto wa Ami ya Mtume wa Mwenyezi Mungu  
aliye mbora kuliko bwana wa viumbe, kiongozi wa  
Hashimiya.**

يا قدوة الدين يا فرد الزمان أصلح لمدح مولى يرى تفضيلكم دينا

**“Ewe kigezo cha dini, ewe mpweke wa zama, sikiliza wasifu, Maula anaona kuwatukuza nyinyi ni dini.**

هل مثل سبقك الإسلام لو عرفوا وهذه الخصلة الغراء تألفينا

**“Je kuna mfano wa kutangulia kwako katika Uislam? kama wangejua, hili ni jambo tukufu tumelipata.**

**هل مثل علمك إن زلوا وإن وهنوا وقد هديت كما أصبحت تهدينا**

**“Je kuna mfano wa elimu yako, hata kama watapotea au watadharau? Na umeshaongoa kama ulivyokuwa ukituongoa.**

هل مثل جمعك للقرآن تعرفه لفظاً ومعنى وتأويلاً وتبييناً

"Je, kuna mfano wa kukusanya kwako Qur'ani unaoujua?  
Kilafidh, kimaana, kitaawili na kiubainifu?

هل مثل حالك عند الطير تحضره بدعة نلتها دون المصلينا

"Je, kuna mfano wa hali yako kwenye ndege, alipohudhuria  
kwa wito alioupata bila kuwahusu wengine wenye kuswali?

هل مثل ذلك للعاني الأسير وللطفل الصغير وقد أعطيت مسكنينا

"Je, kuna mfano wa hayo kwa mja aliyechukuliwa mateka?  
na mtoto mdogo? na bila shaka umeshampa maskini.

هل مثل صبرك إذ خانوا وإذا خبروا حتى جرى ما جرى في يوم صفينا

"Je kuna mfano wa subira yako pale walipofanya khiyana  
na walipotoa habari, hadi yakatokea yaliyotokea katika  
Siku ya Siffini.

هل مثل فتواك إذ قالوا مجاهرة لولا على هلكنا في فتاوينا

"Je kuna mfano wa fat'wa zako pale waliposema wazi:  
Kama si Ali tungeangamia katika fat'wa zetu.

يا رب سهل زياراتي مشاهدهم فإن روحني تهوي ذلك الطينا

**"Ewe Mola wangu Mlezi! nifanyie wepesi niweze kuzuru sehemu zao takatifu, kwani roho yangu inaupenda udongo huo.**

**يا رب صير حياتي في محبتهم ومحشري معهم آمين آمينا**

**"Ewe Mola wangu Mlezi! yajaalie maisha yangu katika mapenzi yao, na ufulufuo wangu uwe pamoja nao. Amin, amin.<sup>49</sup>**

---

<sup>49</sup> *Al-Manaqib*, Muasasatul Balagha Beirut chapa ya 2005 Sura ya Uk.103.

---

## MWISHO

---

Na kwa haya inatubainikia haki ya Imam Ali (a.s.) katika upande wa kuwa kwake mjuzi zaidi kielimu, kifikihi na kujua kwake hukumu, na pia kukiri kwa Makhalifa juu ya hilo. Na katika mistari hii michache tunabainisha haki ya Amirul-Mu'minina (a.s.) kwa ukhalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kama ambavyo tunataka kuwabainishia watu umuhimu wa kuchapisha vitabu vya Aqaidi (itikadi) na kuvisambaza ili kuelimisha wafuasi wa Ahlul-bait (a.s.), na kuwafahamisha wale waliokhalifu madhehebu haya matukufu ya Ahlul-bait (a.s.) na Maimamu wetu (a.s.), na hili ni jambo la dharura na muhimu kwa ajili ya kueneza Ushia, kwani Ushia ndio njia ya haki na sahihi ya Uislamu, hivyo ni wajibu wetu tuzingattie kusambaza vitabu, kuvichapisha na kuvieneza, kwani sisi tuna kiu mno ya fikra. Watu hawawajui Ahlul-bait (a.s.), hiyo ni kwa sababu ya kusambaa fikra za Bani Ummaya, na kukandamiza kwake njia mbalimbali za Kiislam. Hivyo kuchapisha vitabu ni njia bora zaidi kuliko kutuma mali nje, kwani vitabu ni sadaka yenye kudumu kama ambavyo vitabu vinafanya kazi ya kuelimisha akili na kuelimisha jamii na kuhuisha jambo la Ahlul-bait (a.s.), kama ambavyo kuchapisha vitabu ni bora zaidi kuliko kuchapisha picha za wale am-bao wanawaitakidi kuwa ni Marja'a wao.

Unakuta katika nyumba zao picha 1631, katika gari na katika mkoba, wanazichovya picha zao dhahabu kana kwamba wanamwabudu mwenye picha hiyo – Audhu-Biillah - au kana kwamba ni mnaswara ambaye ana msalaba mkubwa wenye kuning'inia kifuani kwake, wakati ambapo yeye

ameghariki katika ufulusuka na uovu, hawa hawajui mambo mepesi ya kififihi, aqaidi, lakini wao kwa kasumba ya ujahili wanatundika picha, hivyo hatimaye wakapotosha Ushia na wakayapaka matope madhahebu ya Ushia kwa ujinga wao.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mjuzi atuimarishe katika madhehebu ya Shia Al-Imamiya Al-Ithna Ashariya, na atupe tawfiq ya kuwatumikia Ahlul-bait (a.s.) kwa kusambaza vitabu ambavyo vimepokea fadhila zao kwa sanadi sahihi, na tunamuomba Mwenyezi Mungu atukubalie haya machache kwa Qabul nzuri, kwa baraka za Sala na Salamu za Muhammad wa Ali Muhammad. Na tunawataka radhi ikiwa katika kitabu kuna makosa au upungufu wowote, sawasawa uwe wa uchapishaji au wakilugha.

*Wanas'alukum du'a,*  
Mwenyezi Mungu awape tawfiqui.

**Ahmad Mustafa Ya'qub**  
**Al-Kuwait 21 / 1 / 2008**

**Kwa mawasiliano na mtunzi tumia:**  
**Barua Pepe: Tanwerq8@hotmail.com**

---

## BIBLIOGRAFIA

---

1. Ibnu Hanbal – Ahmad bin Hanbal: *Fadhalus-Sahabah*. Kimehakikiwa na Wasiyullah bin Muhamda Abbas daru Ibnu Al-Jauziy – Al-Mamlakatul Arabiya Saudiyah, chapa ya tatu 426A.H.
2. Anasay - Ahmad bin Shuaibu: *Khaswais Amirul-Muuminina Ali bin Abi Talib (r.a)*. Kimehahakikiwa na Abu Abdallah Al-Amily As-Salafiy Ad-Daniy bin Munir Al-Zahary Al-Maktabatu al-Asiriyah, Beirut.
3. Al-Hakim Anisabury – Muhammad bin Abdillah: *Al-Mustadrak Alas-Sahihain*. Kimehakikiwa na Hamdiy Ad-Damardash Muhmmad Al-Maktabat Al-Asriya Berut-2006.
4. Ibnu Taimiya - Ahmad bin Abdul-Halim bin Abdusalam: *Al-Istiqamah*. Kimehakikiwa na Ahmad Jaad. Darul-Hadith Cairo 2005.
5. Ibnu Taimiya - Ahmad bin Abdul-Halim bin Abdusalam: *Al-Imanu Al-Awsat*, Dar Ibnu Hazim – Beirut – Chapa kwanza 2003.
6. Ibnu Taimiya - Ahmad bin Abdul-Halim bin Abdusalam: *Radu Alal-Akhinay Qadhil-Malikiyah*. Kimehakikiwa na Dar Ibni Muniry Al-Zahawiy Al-Maktabat Asriya, Beirut Chapa ya kwanza 2002.
7. Al-Khawarizimi - Al-Muwafaq bin Ahmad Al-Makiy: *Maqtalul-Imam Husein (a.s.)* – Dar Anuwaril- Huda – Qum chapa ya kwanza 1418.

8. Khawarizimiy - Al-Muwafaq bin Ahmad Al- Makiy: *Al-Manaqib*, Muasasatul – Balagha, Beirul – chapa kwanza 2005.
9. Tabariy - Abu Ja'far Ahmad: *Riyadhun-Nadhar Fiy Manaqib Al-Asharati Al-Mubashirina bil-Jannah*, Dar Naduwa Al-Jadid - Beirut chapa kwanza 1998.
10. Al-Kanjiy Ashafiy - Abu Abdillah Muhammad bin Yusuf Al-Qarashiy: *Kifayatut-Talib Fiy Manaqib Ali bin Abi Talib*, Sharkatul-Kutubiy, Beirut Chapa ya nne 1993.
11. Ibnu Qutaybah Ad-Diynury – Abdillah bin Muslim: *Al-Imamah Wassiyasah* – Darul-Kutubil – ilimiyah – Beirut Chapa pili 2006.
12. Abiy Ya'li Al-Muswiliy - Ahmmad bin Ali bin Al- Muthana Atamimiy: *Musnad Abi Yaaliy Al-Muuswily*. Kimehakikiwa na Husein Saliym Asad, – Darul – Maamun lil-turath – Damascus chapa ya pili 1989.

---

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION**

---

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swalaa
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu

21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
- 39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyga
46. Kusujudu juu ya udongo

47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini

72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa

97. Sadaka yenyewe kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru

123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu

172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na kujituma ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Weledi juu ya Mustakabali
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa

---

## **KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA**

---

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

---

MUHTASARI